

BENKI KUU YA TANZANIA
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Simu: +255 22 223 3167

Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz



BANK OF TANZANIA
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
TANZANIA

Phone: +255 22 223 3167

Email: botcommunications@bot.go.tz

21 Juni, 2023

TAARIFA KWA UMMA

NI MAKOSA KUJIHUSISHA NA BIASHARA NDOGO ZA HUDUMA ZA FEDHA BILA LESENI YA BENKI KUU AU TAASISI ZILIZOKASIMISHWA MAJUKUMU HAYO

Benki Kuu ya Tanzania imebaini kuwa kuna baadhi ya taasisi, kampuni na watu binafsi wanaojihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila ya kuwa na leseni, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Aidha, taasisi, kampuni na mtu binafsi wasio na leseni hawaruhusiwi kufanya biashara ya kukopesha. Kufuatia kifungu cha 16(2)(a) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, hatua zitakazochukuliwa kwa ukiukaji wa Sheria hiyo ni pamoja na faini isiyopungua Shilingi Milioni 20 au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili.

Benki Kuu ya Tanzania inawakumbusha watoa huduma ndogo za fedha waliokwisha kupata leseni kufuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania ikiwemo kuwapa wakopaji mikataba, kuonyesha riba ya mkopo kama ilivyopitishwa kwenye sera ya mkopo, gharama nyingine zote wanazotoza, na riba kukokotolewa kwa mwezi na sio kwa siku.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuwaasa wananchi kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambao hawana leseni. Aidha, orodha ya taasisi, kampuni na watu binafsi wenye leseni za biashara ya kukopesha zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania inapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu ambayo ni www.bot.go.tz na kwenye matawi yake yote.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:

Kurugenzi ya Usimamizi wa Sekta ya Fedha Idara ya Usimamizi wa Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, S.L.P 2939 Dar es Salaam Simu Na. +255-22-223-5585; Barua Pepe: info@bot.go.tz or botcommunications@bot.go.tz

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA